# LINEA: Utafiti wa Mafunzo juu ya Mila, Unyonyaji na Ukatili kama Njia ya Kuzuia Ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima Mwanza, Tanzania

JOYCE WAMOYI, NERISSA TILOUCHE, MARJORIE PICHON, VERONICAH GIMUNTA, REVOCATUS SONO, ANA MARIA BULLER

## UTANGULIZI

- Ngono za kubadilishana zawadi kati ya watu wanaotofautiana kiumri hupelekea matokeo mabaya katika afya ya uzazi, kiuchumi na kijamii, hi inajumuisha VVU, mimba zisizotarajiwa, utoaji mimba usio salama, kuacha shule, ndoa za mapema au za kulazimishwa na ukatili[1].
- Wasichana balehe na wanawake walio katika umri mdogo wanachangia kwa asilimia 32% ya maambukizi mapya ya VVU katika eneo la Mashariki na Kusini mwa Afrika, licha ya kuwa kundi hili la watu ni takriban asilimia 10% tu ya watu wote, na wana uwezekano wa kuambukizwa VVU mara 2.5 zaidi ya vijana balehe na wanaume walio katika umri sawa na huo[2].
- Kuna ushahidi mdogo wa kitakwimu kuhusu kitu kinachoweza kuzuia ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima. Mpango wa LINEA ni afua ya kwanza iliyojidhatiti kuzuia uwepo wa ngono za aina hii kama lengo lake la msingi.
- Utafiti huu utachangia kutika kongeza ushahidi wa kitakwimu kimataifa juu ya namna ambavyo vyombo vya habari vyenye kutoa burudani vinaweza kutumika katika kuzuia na kupunguza ukatili wa kijinsia, hasa kwa makundi ambayo ni vigumu kuyafikia au pale ambapo utekelezaji wa njia ya ana kwa ana inapokumbana na changamoto.

## AFUA YA LINEA

LINEA ni afua iliyoandaliwa kwa kutumia ushahidi wa kitakwimu, iliyotayarishwa kwa ushirikiano na kufanyiwa upembuzi yakinifu ambayo inalenga kuzuia ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima kwa kulenga mtu mmoja mmoja lakini pia desturi za kijamii kwa kuwalenga wasichana na wanaume[3]. Afua hii tayari imekwisha kufanyiwa utafiti katika mikoa ya Shinyanga na Kigoma na kuleta mafanikio mazuri sana[4]. Afua hii inajumuisha mambo mawili:

### IGIZO LA REDIO LIITWALO MSICHANA WA KATI

Igizo la redio lililo na sehemu 39 (litakalorushwa kila wiki) Linalohusiana na masuala ya ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima Kupitia simulizi za maigizo ya redioni, wasikilizaji watapata kufahamu tabia na kushuhudia jinsi watakavyoweza kusaidiana kuchukua hatua ili kuepuka na kuzuia ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima.

- Walengwa: Wanajamii wote
- Idadi ya sehemu katika igizo la redio: Sehemu 39
- Urefu wa kila sehemu: Dakika 15-20
- Idadi ya washiriki: Wanajamii wote
- Muda: Miezi 9

### MTAALA WA WASICHANA NA WANAUME

Mtaala huu utafundishwa kila wiki kwa zaidi ya wiki 17 kwa wasichana balehe (wenye umri wa kati ya miaka 13-15) na wiki 18 kwa wanaume (wenye umri wa miaka 23-50), pamoja na igizo la redio. Mtaala umeundwa ili kuwezesha mabadiliko katika maisha ya washiriki katika ngazi ya mtu mmoja mmoja pamoja na desturi za jamii zao, kwa kuhimiza tafakari za kina juu ya masuala ya kijinsia, uwezo na maadili ya mtu binafsi. Mtaala unazingatia zaidi desturi mbadala na mafanikio ya malengo kwa wasichana.

- Walengwa mahususi: Wasichana wa umri balehe miaka 13-15 na wanaume wa mika 23 na zaidi
- Idadi ya vipindi: Vipindi 17 kwa ajili ya wasichana na vipindi 18 kwa ajili ya wanaume
- Urefu wa vipindi: Dakika 90 kwa wasichana na dakika 120 kwa wanaume
- Idadi yawashiriki: 15-25
- Muda: Miezi 4

Michoro ya wahusika wa igizo la redio la Msichana wa Kati






## MALENGO YA UTAFITI

Utafiti huu unatumia mbinu ya majaribio. Utafiti huu unalenga kutathmini matokeo kwa kutumia igizo la redio peke yake ukilinganisha ukitumia igizo la redio pamoja na Mtaala kwa lengo la kuzuia ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe wenye umri kati ya miaka 13 hadi 15 na wanaume watu wazima wanaowazidi wasichana kwa Zaidi ya miaka 5 hadi miaka 10 katika mikoa ya Mwanza na Geita. Yafuatayo ndo Malengo mahususi:

1. Kufanya tathminini ya matokeo ya muda mfupi na muda wa kati ya utekelezaji wa (1) Igizo la redio pamoja na warsha ya Mtaala wa wasichana na wanaume katika vikundi vya watu wachache (2) Igizo la redio pekee, kuhusu desturi za kijamii zinazopelekea kuwepo kwa ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima wenye tofauti za kiumri pamoja na tabia za kutoa zawadi kama njia ya inayopelekea kuwepo kwa ngono ya kubadilishana zawadi kati ya wasichana balehe na wanaume watu wazima.
2. Kufanya tathminini ya matokeo ya muda mfupi na muda wa kati za kuhusu kuenea kwa jumbe muhimu kutokana na utekelezaji wa igizo la redio na mtaala miongoni mwa wanakaya na vijana wengine wenye rika sawa na washiriki wa utafiti huu katika jamii iliyolengwa, na jinsi gani kuenea kwa ujumbe huo umetokana na na ujumbe ulioingizwa katika vikundi vinavyotumia mtaala.
3. Kupima ni kwa namna gani mazingira ya utekelezaji (kwa mfano mitizamo na desturi za watekelezaji, muundo wa afua yenyewe na tabia zake) yanaboresha au kuathiri utekelezaji wa shughuli za afua katika vikundi vinavyotumia mtaala.

## MPANGILIO WA MUDA NA HATUA ZINAZOFUATA

Afua ya LINEA inatarajia kutekeleza utafiti wa majaribio kati ya mwaka 2023-2026. Ikiwa kutakuwa na matokeo chanya, tunatarajia kushirikiana na wadau wengine ili kueneza zaidi utekelezaji wa afua hii ili kuongeza idadi ya maeneo yatakayofikiwa na vile vile kufanya mabadiliko mbalimbali kwa ajili ya kufikia makundi mbalimbali ya watu ndani na nje ya Tanzania.

## WADAU

- Amani Girls Home (AGH): Wanafanya utekelezaji
- National Institute for Medical Research (NIMR): Wanafanya tathmini
- London School of Hygiene & Tropical Medicine (LSHTM): Wanafanya uangalizi na kutoa msaada wa kitaaluma

## VIONGOZI WA UTAFITI

- Dr Joyce Wamoyi, NIMR Mwanza
- Dr Ana Maria Buller, LSHTM

## WAFADHILI

- OAK Foundation
- Wellspring Foundation

LONDON SCHOOL of HYGIENE &TROPICAL MEDICINE

MACHAPISHO YA REJEA

1 Tener D. (2019). Money, status, love, and death: sexual relations with considerably older persons in African societies—a systematic review. Trauma Violence Abuse. 22(3):527–40. https://doi.org/10.1177/1524838019869092
2 UNAIDS. UNAIDS Data 2021. Geneva, Switzerland: Joint United Nations Programme on HIV/AIDS (2021). Available from: https://www.unaids.org/sites/default/files/media_asset/JC3032_AIDS_Data_book_2021_En.pdf
3 Howard-Merrill, L. Pichon, M., Sono, R., Riber, J., Wamoyi, J., & Buller, A.M. (2022). Evidence Brief 3: LINEA intervention development process. Available from: https://www.lshtm.ac.uk/sites/default/files/2022-03/LINEA%20brief%203_FINAL.pdf
4 Pichon M., Carter D.J., Howard-Merrill L., Sono R., Gimunta V., Rutenge O., Thiaw Y., Stoebenau K., Perrin N., & Buller A.M. (2022). A mixed-methods, exploratory, quasi-experimental evaluation of a radio drama intervention to prevent age-disparate transactional sex in Tanzania. Frontiers in Reproductive Health. 4:1000853. https://doi.org/10.3389/frph.2022.1000853.